

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

(CKRC)

VERBATIM REPORT OF

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,

KEIYO SOUTH CONSTITUENCY, HELD

AT TAMBACH TEACHERS TRAINING COLLEGE

ON

3RD JULY 2002

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, KEIYO NORTH CONSTITUENCY
AT TAMBACH TEACHERS TRAINING COLLEGE
HELD ON 3RD JULY, 2002

Present

Com. Domiziano Ratanya
Com. Riuinga Raiji
Com. Salome Muigai

Secretariat in Attendance

John Watibini	-	Programme Officer
Lynne Sigei	-	Asst. Programme Officer
Grace Gitu	-	Verbatim Reporter
Francis Kigen		District Co-ordinator

The meeting was called to order at 10.35 a.m. with Com. Ratanya on the Chair.

Francis Kigen: We are ready now to start, and while we wait for other people to come, we will go ahead and start hearings for today. But before that, I would like to call upon Mrs. Sumbeiywo to lead us in a word of prayer, and then, I will hand over to the Principal to welcome our guests – Commissioners of CKRC and District Commissioner to welcome them, and then we leave them for the business of the day.

My name is Francis Kigen, I am the District Co-ordinator – Keiyo.

Mrs. Selina Sumbeiywo: Na tuombe. Baba katika jina la Yesu, tunakuja mbele yako asubuhi hii njema, tukirudisha sifa na utukufu kwako Mungu wetu. Asante Jehovah kwa ajili ya safari njema ambayo umewapa Commissioners ambao wamekuja kuwa pamoja nasi siku ya leo Jehovah. Tunakushukuru Mungu kwa ajili ya siku hii. Hii ni siku ambayo umeteua katika District yetu Jehovah, hili hata nasi tuweze kupeana maoni yetu kwa ajili ya Constitution ya Kenya, Jehovah. Katiba ilikuweco Jehovah, hata wewe Mungu ulitoa amri zako, na hiyo ndio amri ambayo tunatembea tukiwa nayo hata wakati huu Jehovah. Na hata kila nchi Baba, umeteua wakuwe na Katiba yao Jehovah ambayo itasimamisha nchi. Hatutaona hii ni kitu kigeni kwetu Jehovah, lakini, bali tunajua, ilitokana na wewe. Jehovah, nchi ya Kenya tunakabidhi mikononi mwako, hili na mapenzi yako Baba iweze kutendeka. Baba tunahitaji nchi ambayo itakuwa ni vyema kwa kila mtu Jehovah – kwa wale wazee, kwa waume, kwa wake, kwa watoto, na hata wajane, na hata yatima, Bwana. Tunahitaji nchi Bwana, ambaye itawezesha kila mtu kukaa vyema kulingana na mapenzi yako Jehovah. Baba, asubuhi ya leo, tunakabidhi yale yote ambayo tunaenda kunena asubuhi hii njema mikononi mwako Jehovah hili mapenzi yako ipate kutendeka. Baba, anza pamoja nasi, na ukamilishe pamoja nasi. Tukimaliza Jehovah, sifa na utukufu itakurudia Baba, kwa sababu nimeomba katika jina safi la Yesu Kristo aliye Bwana na Mwokozi wetu. Amen.

Principal (Tambach TTC): Com. Salome, Com. Irungu, Com. Ratanya, the DC – Keiyo, officials of Keiyo Review Commission, wananchi watukufu, good morning?

On behalf of the College, I would like to welcome the Commissioners very sincerely to our institution, and we ask them to feel free and enjoy the use of these facilities, the whole day, and they are even welcome to stay, if they want to stay over-night – we have rooms in this College where we can accommodate you Commissioners.

Wananchi I also welcome you to your college, please feel free, give views, be effective in the discussion. I want to wish you luck as you deliberate on these important issues touching on our lives, touching on our nation. I want to say that, even the college students prepared documents. They will present something, “wapi a student”? A government of students is also here -- that is an ex-student, a councillor, he is called Cllr. (inaudible), Bwana Mones, sema amechukua kiti chako, Bwana councillor (inaudible).

So, with those few remarks, let me welcome the DC to continue with the rest. Bwana DC, welcome.

DC, Keiyo: Thank you very much our Senior Principal, our Commissioners, Ladies and Gentlemen, I wish to take this opportunity to welcome you on behalf of our leaders in this District. Although you may see that we are few, but what has happened Commissioners is that, people have made write-ups, which I think is going to make your work very easy. I know

that when you came, you were not sure whether the District Headquarters is in Tambach or in Iten. Prior to 1973, this used to be our district headquarters, but currently, we are up in the highland in Iten, where you will be tomorrow, in the county council hall.

Ladies and Gentlemen, the business of today, this is why you find we didn't want to put chairs here. I am going to sit with you, and listen to what you are going to present. But just before I hand over, personally, as a Kenyan, there are issues that really we must take into account and we must retain in the Constitution.

One, is the court of arms: the court of arms is a very important instrument and sign of unity for all of us.

The Kenyan flag: must also be taken into account, and I wish to propose that this must also be retained.

On issues of local authorities: I have sat in local authorities for many years, I wish to propose, to say that our councils, they need also to be considered, we don't have very many, at least to get some funds from the consolidated funds. Just like our honourable Members of Parliament.

Lastly, but not least, I know I have written a paper, and already it is there, that, we in the provincial administration, alone set-up, is a very important linkage between our people at the grassroot. Right from that village elder, the things that, that village elder can do, but myself, as a District Commissioner, I am not able to. So, right from those elders, must be retained in this Constitution, because, I have said – I am saying that because, the administration of today, is not the administration of the 70s. All that we do at the moment, we do development administration.

Ladies and Gentlemen, you are most welcome. The Commissioners, feel free, I know you have been with us for three days. Our Member of Parliament for this constituency – this is the Keiyo North Constituency, will not be able to be with us. But, he has sent in his suggestions.

So, with those few remarks, you are just welcome. I wish also to say, that security in this district where I am as the chairman of the District Security Committee, it is (inaudible). I was only saying that, security of our properties and our lives, should not be left with us. It should be in the hands of each one of us, so that when we talk about the cattle-rustling, I also keep on asking myself, our neighbours, if they finish those animals, and they have the guns, what is going to happen? This is an issue that must be looked into very carefully, by all of us, by talking to our people, so that behavioural change must actually, be changed, that people are taken to school.

As I said last but not least, Commissioners, I am gender-sensitive. Issues on rape, if any man commits rape, I would say, I think that fellow should be hanged. Thank you.

Com. Ratanya: Bwana DC wa Keiyo District, Deputy Principal wa College hii, Co-ordinator wa District hii, katika Constitution of Kenya Review Commission, Wananchi wa hapa Keiyo North Constituency, hamjamboni nyote?

Response: Hatujambo.

Com. Ratanya: Kabla hatujaanza, tungetaka kujuana. Kwa sababu munatuona hapa, tuko mbele hapa, na viongozi wengine, hatujajuana. Kwa hivyo, hiyo introduction ingekuwa pengine kitu cha kwanza. Na Co-ordinator, pengine una ile committee yako ambayo inaendesha, munasaidiana nayo. Pengine ukianza hapo, ingekuwa mzuri, halafu tuendele.

Francis Kigen: Okay, asante Chairman Commissioner. Nafikiri nitaanza na Chairman wa Constituency Committee – Bwana Lucas Chepkotong. Yeye ni Chairman ya Constituency Committee, Keiyo North. And may I ask other members who are present to stand up. My two ladies, Mr. Francis Cheplait over there, he is a CCC member. Then we have here, Maurice Tuton, and then we have Mrs. Selina Sumbeiywo. Thank you. The others are busy – that is, Julius Kiprop over there at the gate, manning the gate. The others are busy organizing for tomorrow's session. Thank you.

Com. Ratanya: Okay, asante Bwana Co-ordinator, hapa hata sisi tuna staff wetu, ingawa hawa munaona hawa ni Commissioners ambao nitawajulisheni kwa nyinyi. Lakini kwanza, ningetaka mujue, watu ambao tunasaidiana nao. John Watibine endelea hapo. Huyu John Watibine ndiye kiongozi wa hao wengine ambao tunao. Pale unaona Recorder wetu – Grace.

Grace Gitu: Hamjambo?

Response: (inaudible)

Com. Ratanya: Na huyu msichana mwingine Sigei. Unaona hata dereva wetu, kuna mmoja hapa anaitwa Maingi, kuna mwingine pale Kamau, na mwingine pengine yuko nje anaitwa Abraham ambaye hayuko hapa.

Na kutoka hapo, sasa ni Commissioners ambao tunao hapa ambao munaona mbele hapa. Upande wangu wa kulia, tuna Com. Salome Muigai, na upande mwingine, tuna Com. Riunga Raiji, na ningetaka kila Commissioner pengine asalimie nyinyi na ajiulishe yeye mwenyewe kabla hatujaanza. Tuanze na Com. Salome.

Com. Muigai: *Change tugun?*

Response: (inaudible)

Com. Muigai: Tuna furaha sana kuwa hapa na nyinyi, na ninafurahi sana kuona kina mama na kina baba, tuje tuzungumzie hii

hali yetu ya Katiba yenye tungetaka. Karibuni.

Com. Raiji: Hamjambo ndugu na dada zangu?

Response: (inaudible)

Com. Raiji: Kama mumesikia, mimi naitwa Riunga Raiji, na ni furaha yangu kuwa na nyinyi siku ya leo. Asanteni.

Com. Ratanya: Na mimi ambaye niko kati kati hapa, jina langu, naitwa Domiziano Ratanya, ambaye vile vile ni mwenyekiti wa kikao hiki ambacho tuko nacho hapa siku ya leo. Hamjamboni tena?

Kutoka sasa, saa hii, tumetangaza hiki kiwe kikao cha Tume ya Kurekebisha Katiba ya Kenya. Na kabla hatujaanza, ningetaka niwajulishe mambo machache ambayo tutafuata. Kitu cha kwanza, tumeandika list hapa, wale ambao wamekuja wameandikishwa, na tutajaribu kutumia hii. Yule wa kwanza kuingia, ndiye tutaita akiwa wa kwanza na kuendelea namna hiyo.

Lakini kukiwa kuna sababu yeyote ya kuita mtu, hata watano ama kumi, nitafanya hivyo, kwa sababu, munajua kama mama akija mzee sana, ama mwanaume akija mzee sana, ambaye hawezi kukaa hapa, wa miaka kama 80 hivi ama 90, lazima tumusikie huyo, hili aende kufanya kazi ingine, asije akachoka. Na kama mama akija hapa ambaye tunamwona ya kwamba hawezi kungoja, na ni lazima tumupatie nafasi, hata hiyo tunamupatia nafasi. Tena kukiwa na mwanafunzi, ambaye ametoka kwa class, na tungetaka apeane maoni yake, halafu arudi kwa class, hapo nitatumia mamlaka hayo kumukubali aende katika class. Kwa hivyo hayo machache ndiyo tutafanya. Otherwise, tutatumia hii, “first come, first served”. Hiyo ni kitu ya kwanza nilikuwa ninataka mujue.

Kitu kingine ni kwamba, wakati munakuja hapa kupeana maoni yenu, mtu akiwa na memorandum ama maandishi ambayo umeandika, umeandika pengine kwa Kiingereza, Kiswahili, sijui pengine hata kwa lugha yako, hayo maandishi, hatutakubalia wewe uendelee kusoma, kwa sababu ukiendelea kusoma, utakaa karibu saa moja, na utapoteza wakati wa wale wengine ambao wangetaka kusema.

Ukiwa na memorandum, kuna njia mbili. Njia ya kwanza, utapeana pale iandikishwe, bila kusema lolote, uiache, ukitaka kuketi hapo usikilize wengine, ni sawa sawa. Ukitaka kwenda, unaenda. Ama, ukiwa na memorandum, na unataka kuitetea kidogo, utapewa hiyo dakika tano, to highlight. Yaani kusema yale ya muhimu. Point, point, ile ya muhimu tu. Sio kusoma memorandum. Ni point ya muhimu, halafu unatupatia memorandum hiyo. Kwa sababu tutakuwa na nafasi nyingi sana uko katika headquarters yetu Nairobi kusoma. Na tuna watu wa kusoma na kujua yale yote umeandika. Kwa hivyo hapo, ni kusema yale ya muhimu, na kupeana hapo, na utumie hiyo dakika tano ambayo nitakupatia.

Na tena, ukiwa huna maandishi yoyote, wewe unataka tu kuzungumza kwa mdomo, mambo ambayo yatakuwa kwenye kichwa

chako. Kwa hivyo utakubaliwa, uzungumze, na utapewa dakika tano.

Na wakati unapozungumza, ujaribu kutumia hiki kipaza sauti, na hata hii yenyewe ni record. Inapeleka mpaka kwa recorder, mambo yale unasema yanawekwa pale. Ndio utaona wakati mwingi tutakuwa tunakwambia tumia hii. Si kwa sababu ya sauti peke yake. Ni yale maneno unasema yataenda kwa machine yetu hapa. We are recording. Kwa hivyo utumie hicho.

Ingingine, ni lugha. Lugha ambayo unaweza kutumia hapa, kama unaweza kutumia Kiingereza ni sawa sawa, Kiswahili ni sawa sawa, na hata lugha ya mama, kaka hujui Kiswahili na Kiingereza, umekubaliwa kutumia lugha ya hapa, na tutakuwa na watu wa kutueleza.

Then, ningetaka kuwajulisha kwamba, hiki kikao ni cha Tume ya Kurekebisha Katiba. Na kiko free – yaani uko uhuru, kusema yale ungetaka kutuambia. Usiogope, usiseme kwamba, pengine bwana yako uko nyumbani atakupiga, pengine kama ni mzee atapigwa na bibi yake uko nyumbani, ama utapigwa na mwingine, usiogope. Kwa sababu uko uhuru kusema yale yote unataka kutuambia ya kurekebisha Katiba hii yetu ya Kenya. Uko uhuru. Kwa hivyo, usiogope.

Tena, ningetaka kuwajulisha kwamba, niwambie tena mambo ya masaa. Nitakupatia dakika tano kwa mambo yoyote yale utasema. Ukiwa na oral presentation, dakika tano, ukiwa na memorandum na utasema yale ya muhimu, dakika tano. Kwa hivyo usingoje, nikuambie kila wakati, stop, dakika imekwisha, kila wakati. Hata wewe tumia saa yako. Dakika tano ikiisha, ama kama unataka kuongea kama dakika tatu ama nne, tano ikifika, umalize, na uende pale, u-sign register yetu, na upeane memorandum yako hapo. Usinifanye kama chairman niwe nakuambia, eeh, saa imekwisha, saa imekwisha, tutakubaliana hivyo. Nimesema hivyo kwa sababu, wale wanataka kupeana mambo yao ni wengi, na hatutaki kukaa hapa mpaka usiku. Tuheshimu saa, saa yako ikiisha, unaenda, mwingine anaingia.

Na sasa, bila kupoteza wakati mwingi, ningetaka tuanze, na kabla ya kuanza, kitu kingine ni kwamba, kama Commissioner – sisi watatu, yeyote ana swali, kama ya clarification ama ukitaka kufafanuliwa kitu fulani, sisi hapa tutakuuliza kabla ya kwenda ku-sign register. Kwa hivyo, ujue hiyo itatokea.

Na ningetaka sasa tuanze straight away, na mtu wa kwanza ambaye ni Abraham Chemolo. Abraham Chemolo, ni wakati wako sasa.

Cllr. Abraham Chemolo: First, Commissioners

Com. Ratanya: Jina.

Cllr. Abraham Chemolo: Jina langu ni Cllr. Abraham Chemolo. Commissioners, Bwana DC, members who have come

here, I wanted to talk – I wanted to present my memorandum for Keiyo Valley Pastoral Community.

Commissioner sir, the Constitution – we as the pastoral community of the Valley, we are people who are living in one of the semi and arid areas, comprising 65% of the Kenya land. We as the community, have been depending on NGOs for a long time. This time, we would like to be included in the Constitution, so that we are given free education.

Also, in that particular area, we don't have health facilities as other areas have. We also want the coming Government to consider building more dispensaries and health centres in these particular areas.

Sir, we also have no infrastructure: we have no electricity for vision in that particular area. We want the same to be included, so that we enjoy the freedom of the country.

Commissioner sir, we also need enough security for the protection of human life. Especially the area where I come from, it is an area where cattle-rustlers are very rampant in the area.

Sir, in addition to that, we want chiefs and assistant chiefs to be elected by the community.

Also, we would like the village elders to be recognized and be paid allowances by the Government, as the people who are handling customary laws, and land cases everyday in the village. They are also popular with the villager.

All the natural resources should be under the community around the said location, e.g. forests, game reserves, etc.

I would also like to highlight that, as a councillor, we would like the Chairman and the Mayor of any local authority to be elected by the people.

On the basis of the government, the structure of government we would like to have, is to retain the unitary government and the system be Presidential.

Kenya should have only at least eight political parties. In other words, each province to have at least one party with a maximum of a million registered members, and a national outlook.

Also, councillors should be recognized and their allowances be paid through the consolidated funds.

Also, to add on that, is that, cases related to animal theft be (inaudible). That is to say that, police should not keep anybody in the cells who has a case of animal theft in nature.

Also, we would like five years for two terms to enable a councillor to be pensionable. And Councillors Service Commission to be established in the Constitution.

Also, we need reserved nomination for a councillor and also a Member of Parliament from the pastoral community.

Also, we would like to have provision of piped water for irrigation and domestic use in our area.

Also to have the community be assisted freely from (inaudible) e.g. beans, maize, oils, etc.

Another one, is that, we would like to have certain offices like—KWS should be in the area, so that when there is recruitment of people, they should take into account where the headquarters is stationed. Because right now, those people who are being recruited are from outside the headquarters. So, we would like it put in the Constitution that, in future, KWS should be stationed in the place (in the remote), whereby, the local community can benefit from such things.

Lastly, we also have free natural resources. These natural resources, are our natural resources are. But we would like in the Constitution, in future, that those people who donated the land be compensated, because they have no where to go.

Also, we would like to have..

(Interjection) Com. Ratanya: Sasa, Abraham, na dakika moja, jaribu kumaliza.

Cllr. Abraham Chemole: Okay, sawa. Also, as a pastoral community, we would like also in the Constitution to have a pastoral centre in our area. Thank you.

Com. Ratanya: Okay, asante sana. Ngoja hapo Abraham.

Com. Muigai: Asante sana Bwana Diwani kwa maoni yako. Mimi nina swali moja. Umesema kuwa ungetaka katika Parliament kuwe na Mbunge mteuzi wa kusimamia habari ya pastoralists. Lakini pia ukasema ungetaka kuwa na mteuzi pia Diwani. You also want a nominated councillor, for pastoralists.

Cllr. Abraham Chemole: Yaah.

Com. Muigai: In which county council? I thought the county councils, within the pastoralist area is made of councillors who

are already pastoralists. I want a clarification on that. I can understand the Parliament one, but the nominated councillor is from what area to which county council?

Cllr. Abraham Chemole: That one, I can say, it is now in Keiyo County Council. We are coming from the Kerio Valley, so we need one to be given in the Constitution, so that, they will have to see the interests of those people who are living there. Thank you.

Com. Ratanya: Okay, asante Abraham. Uende pale. Wilson Omonei. Na kwanza useme jina lako.

Cllr. Wilson Omonei: Asante sana Commissioners. Kwa majina, mimi naitwa Cllr. Wilson Omonei. Yangu nilikuwa nimeyaandika, lakini nitataja tu moja moja ambayo yako na points ambazo ningependa kusema.

Kwanza, Chairman, kwa sababu mimi natoka county council, tunachagua Chairman au Mayor. Ningeonelea huyu Mayor achaguliwe na wananchi – kutoka kwa wananchi.

Kitu kingine ambacho mimi naona kutoka kwa hizo points, ni salaries ya councillors, itoke kwa Serikali, sio kutoka kwa wananchi.

Kitu kingine ambayo mimi nimeona, hasa sana, ni Clerks wa Town Councils. Iwe kutoka kwa area kama County Council hiyo, watoe mtoto wao mmoja ambaye atateuliwa kuwa Town Clerk. Kwa sababu tuko na shida nyingi sana, tunapata Clerk ambaye labda anatoka mahali pengine, analeta problems kwa hiyo Council.

Shida ingine ambayo tunaona kama Councils, ni nominated councillor. Nominated councillor asiwe na kiti chochote katika council. Kwa sababu, yeye ni mtu ali-nominetiwa, na asiwe na neno lolote katika council.

Nafikiri Bwana Commissioner, mimi sitakuwa na maneno mengi, ni hayo, labda tu ningengeza moja. Hii ni upande kina mama. Labda pia, kina mama wawe nominated – waangaliwe, hasa kwa area kama hii ya town councils, tumechaguliwa kama wanaume karibu saba, na tunataka councilors saba. Kama ni nomination, wapee mama moja, ili pia awe councillor katika hiyo upande, kwa sababu tuko na shida, ya kina mama katika councils.

Upande wa education: ningeonelea, kwa sababu, labda sisi katika town, iwe mtu ambaye amesoma mpaka form IV, lakini uangalie area zingine kama, county councils, kwa sababu labda hiyo area, huenda kukawa na ... interest ya wananchi iangaliwe pia, kwa sababu huenda ikawa, kuna mtu ambaye anapendwa na wananchi, na pia aangaliwe.

Nafikiri Commissioners, yangu ni hayo tu. Mimi, area hii ambayo muko sasa, ni area yangu, ambayo ni county council. Asante

sana Commissioners.

Com. Ratanya: Councillor, ngoja kidogo.

Com. Muigai: Asante sana Bwana Diwani. Mimi swali langu ni moja, la ufafanusi. Kwanza, umesema kuwa, councillor mwenye atakuwa amechaguliwa, asipatiwe kiti chochote, na asipatiwe jambo lolote la kusema. Halafu, ukafuatia kusema eti, tuteue kina mama kwa councils. Sasa umewanyima mamlaka mzee kwanza, halafu ndio unawapa uteguzi?

Clr. Omonei: Asante sana Commissioner. Nimetaja hivyo kwa sababu, tumekuwa na shida nyingi na nominations katika councils. Unapewa mtu ambaye wame-nominate, labda hata apewe, ulikuwa umeshinda kama councillor, na yeye pia, anaweza kuchaguliwa kama chairman. Hapo sasa, yule ambaye amechaguliwa na wananchi hana nguvu kuliko yule chairman. Na nimetaja upande wa kina mama, kwa sababu, nimesema kwamba, uenda hawa councillors ambao wamechaguliwa, wote ni Wanaume, na upande moja, tunaona kuna upungufu katika upande wa akina mama. So, ningeonelea, kwa sababu wale wamechaguliwa, mama a-nominekiwa katika hiyo council, ili awe hata anaonyesha sura kwamba akina mama wako hapo, kwa sababu tunaona ni shida kubwa sana. Hasa upande wa social services, tukiwa katika councils, upande wa social services inausu sana kina mama. So, ningeonelea upande huo, ingeangaliwa kikamilifu. Asante sana Commissioner.

Com. Ratanya: Nenda pale, hapa ninaona kuna mwanafunzi ama Mwalimu wa Tambach TTC, na angetaka kwenda kwa class pengine. Sammy Kasongo. Sammy Kasongo wa Tambach TTC. Sammy umepewa dakika tano. You don't have to read the whole memorandum, just highlight the main points for five minutes.

Sammy Kasongo: Thank you very much Commissioners. I am just going to highlight a few points, just like you have said.

The first one, the Presidential elections should be held separately from the Parliamentary and civic elections.

Secondly, candidates rejected by the electorate should not be nominated to Parliament.

Thirdly, a third of the Parliamentary seats should be reserved for women.

The Higher Education Loans Board should also launch to teacher trainees in teacher colleges.

The next one is, a trust fund should be established at district headquarters to assist all the bright-needy children to pursue further education.

And the last one, dressing provocatively in public should be punishable by a fine of Kshs.5,000/-. This will reduce the cases of rape due to provocative dressing, especially by ladies.

And last but not least, primary school education should be free and compulsory for all children. Thank you very much.

Com. Ratanya: Kuna swali Sammy.

Com. Muigai: Thank you very much. Mr. Kasongo, I have one or two questions for you. One, is on the trust fund for bright children. Education is a basic right. So, what happens to the children who are poor, but they are not that bright? If we just say that it is for certain children. That is my first question.

My second question is on provocative dressing especially by ladies. What is the responsibility of men towards rape?

Sammy Kasongo: Thank you very much Commissioner. So, concerning the trust fund, especially the needy but bright. You find that some cases in the district may find children who are orphans, however, they may be bright. So, such children should be catered for, by being assisted by pursue education.

Also, those ones who come from poor families, and they are also not so bright, they should just be considered in the same way as those bright ones, because education is a basic right for children.

Secondly, concerning the dressing, rape cases mostly, they come from the desire someone feels with somebody. And this is mostly highlighted mostly by the kind of dress someone would like to put on. So, in such cases, you find a man, or for that matter a rapist, is more driven to that act, when he sees something that actually will provoke him. Thank you.

Com. Ratanya: Okay, asante sana Sammy. Andikisha pale. Sasa ningetaka tusikie sauti ya akina mama. Hata mmoja hivi. Kwanza Mary Cheboi. Uko karibu? Ni wewe Mary Cheboi? Okay, sawa sawa.

Mary Cheboi: Thank you. Jina langu ni Mary Cheboi. Ningependa niwasalimu nyote katika jina la Yesu. Sasa kwa upande yangu, nimekuja kwa upande wa disabled.

First, kuhusu finance: kwa upande wa hii pesa, kuna ile pesa ya NHIF. Tungependa tueleze Serikali kama inaweza kuchagua committee, ile inakuja mpaka District Headquarters, halafu itufikishie hiyo pesa, ndio ifike mpaka reserve, na hata ifike mpaka kwa chief, ndio igawanyiwe kila mtu.

Upande wa education, tunaomba free education for the disabled children, and children with disabled parents.

Medical: tunaomba free medical schemes for the disabled children and children with disabled parents.

Halafu, taxes: tunaomba the government to reduce taxes for the disabled people, so that these disabled people may be able to buy the equipment for themselves. For instance...

(Interjection) Com. Ratanya: Mary, Mary, ngoja kidogo. Hii ushike vizuri. Ukiweka hapa, itakuwa mbaya. Sasa weka ishike vizuri, ili tusije.....

Mary Cheboi: Kwa mfano, artificial legs ndio tuweze kununua, na hata artificial shoes ikuwe cheap. Kwa sababu, unakuta huyu poor person, cannot be able to buy these things.

Halafu, business: tunaomba free licence and town plots to be separated for these disabled people.

Nominations: tunataka vacancy moja ikuwe ya disabled ndio waweze kuwatetea disabled people, na pia the physically and mentally handicapped.

Shelter: tunaomba Serikali watusaidie kutujengea manyumba, kwa sababu, unakuta huyu disabled, hawezi hata kujenga, kufanya kazi hata ya shamba.

Halafu vitu kama toilets. Anything ile inaweza kusaidia disabled kwa public place. Tuwe considered, kwa sababu, unakuta, mara mingi tukienda ma-sherehe, ile kama Jamhuri Day, hatuna namna ya kutusaidia.

Halafu tunaomba tena employment: Serikali ituwekee kando, nafasi kwa sector yeyote ya Serikali. Ya disabled iwekwe kando, ndio isaidie hawa.

Halafu retrenchment: isikuwe kwamba huyu disabled, ama this mentally handicapped person akuwe retrenched kwanza.

Halafu, transport: ingewezekana Serikali iangalie these disabled, hata, wasilipe transport.

Halafu, kama ingewezekana, these vehicles, zijengwe ile iko modernized, ile inaweza kuwa na switch, ndio disabled anaweza kupanda ama ashuke. Ni hayo tu.

Com. Ratanya: Pengine kuna swali, ngoja, Mary kidogo.

Com. Muigai: Asante sana kwa maoni yako Mary. Mimi swali langu ni hili Mary. Umezungumzia habari ya walemavu kama wanashida zenye zimefanana. Ningetaka unieleze kuwa, shida za akina mama wenye ulemavu. Kwani akina mama

wote wanaonekana wana shida? Na walemavu wana shida? Je, ukiwa mama na una ulemavu, shida hizo zenye zinajitunga pamoja, zinakuwa zipi? Umetupa mfano kuwa, disabled wapatiwe nafasi moja kwa nomination. Wakipatiwa hiyo nafasi, unafikiri itaenda kwa mama ama itaenda kwa disabled mwenye ni mwanaume?

Kwa hivyo ningetaka kusikia shida za kina mama wenye ulemavu.

Mary Cheboi: Mama mlemavu, ningesema kuwa awe nominated, kwa sababu, anaweza kuangalia mpaka ndani kabisa ya nyumbani -- ya disabled mother, ama ya disabled child.

Com. Ratanya: Okay, asante sana Mary. Uende pale ujiandikishe. Tena tuende kwa – anayefuata ni Robert Boit.

Robert Boit: Commissioner sir, the document I am to present is still under process, so I am expecting it in a few minutes. So, the next person to come. Thank you.

Com. Ratanya: Okay, ikija, kwa hivyo utapeana pale? Thank you very much. Then, kuna Masaku Nathu Muthui Daniel. Huyu anaitwa Masaku yuko? Mwingine, ni Joseph Rono. Joseph Rono?

Joseph Rono: Commissioner sir, I would like to ask if there is any deaf person here, because we can't know whether there is any deaf person. So, maybe somebody who is having sign language to ask.

Com. Ratanya: Joseph Rono. Wewe unaitwa Joseph?

Joseph Rono: Yaah, I am a disabled person, so I was talking about the disabled. That is why, I was looking for my deaf people (a disabled group).

Com. Ratanya: But for you, you can talk directly.

Joseph Rono: Yes.

Com. Ratanya: Okay, I give you five minutes. Not to read everything, but highlight in short.

Joseph Rono: I know that. Thank you sir. So, what my colleague has said..... (*end of side A*)

Not to discriminate us or either mistreat us, because, others think that the disabled can do nothing. Let me hope that the law will protect us, to give us opportunities of exercising our capabilities. So, we should be given first priority. Whether it is

employment or any other things to be done. Especially in our families, we should not be neglected or put aside. We should be together with other people of Kenya.

So, in summarizing again, we should be treated in a special way (humanly). That means, in building, we should be considered. In telephone booths, we should be considered. Even roads, even sports, all even properties – when dividing properties. Even the Government may consider us when they are looking for landless people. They should put the disabled to be getting land. And also vehicles, driving, we should be considered to get our own vehicles which we might manage to drive.

In (inaudible) affair, we should be given slightly those monies in district level. These are the funds to the districts. At district level, they should consider us.

In education, the other colleague of mine has said something. She has forgotten about sign language. Sign language should be taught in primary schools, especially in hospitals, because deaf people may go to hospital, but they cannot manage to explain how they are feeling.

In examinations: a disabled person should be given more time in doing exams e.g. national exams. Because he might be slow in writing or the other hand is slow or in another way.

Disabled woman: a disabled woman should be given three months maternity leave, because, disability is another thing which makes her to go slowly, not two months.

Another thing is social way: we need the disabled people to be given funds by the Government, at least every month so as to cover his or her basic problems.

Equipment which my colleague has said, should be free of taxation. This will help the disabled avoid going to towns to beg. We should give the disabled something to do. For example, mentally disabled should have houses in the districts where the Government looks after them. This is because, we find people who are able, go and impregnant the mentally disabled people who are in towns and they bear children....

Com. Ratanya: Nimekupatia dakika moja, jaribu kumaliza.

Joseph Rono: So, what I was saying is that, the mentally disabled should have homes in the districts.

So in winding up, I will say that we should be getting free medical services.

About courts, sometimes we are not able to pay the advocates. So, the Government should assist the disabled.

Winding up, there are people who work with the disabled, and they don't get enough allowances. If it is possible, those people who are bringing these people together, because they were neglected, they should earn hardship allowances.

About land, let them get like other people. Thank you very much.

Com. Ratanya: Okay, kuna swali ngoja kidogo.

Com. Raiji: Asante sana Bwana Joseph Rono. Umezungumzia hii mambo juu ya urithi, kwa wale wananchi ambao wasiojiweza. Sasa nauliza, katika mila zetu, tuseme kama hapa, uko ubaguzi wakati tuseme baba anapatia watoto wake mali yake au shamba?

Joseph Rono: Of course, there is, because you find that they think I can do nothing. So, they plough all the shamba without giving me a piece, or even not allowing me to marry sometimes. They think that I cannot look after my children. They don't even like ladies to bear children. They go for contraceptives, making them not bear children.

Com. Ratanya: Swali ingine.

Com. Muigai: Asante sana Bwana Rono, umezungumzia hali ya watoto wenye ulemavu kupatiwa wakati mrefu wakati wa mitihani. Lakini ukuzungumzia juu ya masomo yao. Kwanza, sijui kama kuna shule za kutosha, kama upande huu kwa watoto wenye ulemavu. Ndio hata afikie wakati wa kufanya mtihani. Ni lazima awe tayari, ameshaenda shule, na akasoma. Kwa hivyo ningetaka utueleze juu ya hali ya watoto wenye ulemavu kufika shuleni, kuweza kusoma, hata kufikia ule wakati wa kufanya mtihani.

Na pia habari ya bursaries na vitu kama hivyo vile wanavyouzishwa kwenye eneo hili na vile tungeweza kuwauzisha.

Joseph Rono: Asante sana Commissioner Madam. Hiyo ndio kitu nilikuwa ninaangalia. Tulianza small homes, na funds hakuna – pesa. Na tunaona ya kwamba, kama Serikali wakisaidia pesa – funds (small loans), ama rehabilitations kwa districts kama iko moja moja kwa kila district, halafu disabled waweze..... Kwa sababu mambo ya kulipa, ndio ilikuwa sasa hawalipii disabled, wanalipia able children mostly. Wana wacha huyu, kama si mtu.

Halafu kwa masomo, unajua hawa watu ambao wanafanya na disabled. Wamefanya bidii kuwapatia morale, kuwapatia moyo wa kutaka somo. Sasa wanataka, wengine wamesoma, na school fees imekuwa shida. Kuna moja hana miguu mbili, hana mkono, anaenda university, lakini hakuna funds. Saa hii hako nyumbani.

Na ma-shule haitoshi ya wasiojiweza. So, ndio unaona ma-shule zingine zinajenga gorofa, na disabled awezi. Wanajenga mahali ambapo disabled hawawezi. Kwa hivyo, disabled wapewe nafasi ya kwanza kwa masomo, na pia, kwa mambo ya employment – kuandikwa kazi. Lazima apewe, ajaribu mahali anaweza. Kwa sababu akiambiwa hawezi, anakuwa hawezi, hawezi. Lakini akiambiwa utaweza, anaweza kuwa na moyo wa kuendelea. Asante.

Com. Ratanya: Rono, umemaliza. Mary Ruto.

Mary Ruto: Asante sana. The Presiding Commissioner, being one of the committee member, I have the following to say:-

Com. Ratanya: Your name.

Mary Ruto: My name is Mary Ruto, and I am representing my paper from the elderly and retired persons.

Those married women or engaged in customary law, must receive legal certificates through the Judiciary, facilitated by the council of elders. Ninasema hivi, kwa sababu, kwa wakati huu, wale wameolewa ki-nyumbani, hawana legal certificate, kama wale wameolewa kanisani, na hata wale wamefunga ndoa katika DC's office. Kwa hivyo tungependelea ya kwamba, hata wale wameolewa ki-nyumbani under customary law, wapewe legal certificates.

Another one is that, in case the husband dies, the wife should have full authority and power over the family land and property. Wakati huu, katika Keiyo customs, bwana akifa, kijana mkubwa anapewa jukumu ya kuongoza jamii ama kushika hiyo properties ambazo ziko kwa hiyo familia. Kwa hivyo, tungependelea ya kwamba, mzee akifa – in case the husband dies, the woman should have power over the family land and property.

Another one is, all family assets e.g. land should be inherited by all children – both boys and girls without discrimination. Ninasema hivi kwa sababu, watoto wote wamezaliwa na baba mama, na kila mara katika historia ya Keiyo, ni kwamba, msichana hawezi kurithi mali nyumbani. Kwa hivyo ningependelea ya kwamba, kwa sababu wote ni watoto wa nyumba moja, lazima wapewe inheritance, ama kuchukua jukumu ya kupewa nafasi kurithi hiyo mali.

Another ni kwamba, according to our culture, women were exempted from daily duties for six months after delivery. Hence, it should be included in the Constitution. Kwa wakati huu, ninajua ya kwamba, mama yeyote anafanya kazi katika serikali, uwa anapewa two months maternity leave. Na kweli two months maternity leave, haiwezi kumpa mama nafasi ya kupata nguvu ya kufanya kazi. Kwa hivyo ningependelea ya kwamba, iwe included in the Constitution kwamba, maternity leave iongezwe iwe six months, ili mama apate nguvu.

Nyingine ni kwamba, incest and defilement of minors is a taboo, and persons found breaking this law, were either stoned to death or ex-communicated from the society. And therefore, the Constitution must address this person found guilty, to be given highest penalty. Hii ni kwamba, katika kazi ya ki-Kalenjin, mtu akipatikana kama ame-defile msichana ama amemunajisi mtoto msichana, huwa anapigwa, ama anapigiwa katika shimo. Huwa wanachimba shimo, halafu wanafungia yeye, anakaa overnight, au anapiwa kabisa mpaka afe. Kwa hivyo tunaona ya kwamba hii katika Constitution, huyu mtu apewe highest penalty.

Retirement: pension to be raised, whenever there is an annual salary increment. Pensions wakati mtu anapewa mshahara, au pensions wakati watu wanaongezwa mishahara, wale wame-retire waongezwe pia – that is salary increment.

The accused elderly persons should not be remanded in police cells, unless they have committed, e.g. rape or murder, etc.

The police should not arrest and use the elderly as a base in case they fail to arrest offenders.

Illegal brewers, so to be private or follow it to stations. Ni kwamba police kila mara wakishika watu ambao wameshikwa busaa, wanapeana pesa kabla hawajafika police station. Ni afadhali mtu afike police station, ili ahukumiwe.

Nyingine ni kwamba, children found neglecting their elderly parents must be prosecuted.

Nafikiri ni hayo ambayo niko nayo.

Com. Ratanya: Okay asante sana Mary Ruto. Peana karatasi yako hapo. Kuna Judith Cheruiyot.

Judith Cheruiyot: Okay thank you. Mini na-represent Kenya Women Political Caucus. In Kenya to develop political caucus, it calls for affirmative action, under 35% of seats be reserved for women in Parliament and in all public bodies.

In land and property rights: we call to have the rights to all and inheritance to land, and other movable and immovable properties by women, should be added as a right in the Constitution.

In the cultural, ethnic and regional diversity and communal rights: since culture should not have a fundamental right, and even culture, is dynamic, it can change. So, efforts, through enactment of laws should be made to outlaw harmful, cultural practices and traditions such as female genital mutilation, early and forced marriages.

Also, child rights should be protected, whereby, a child should be defined as a girl or a boy, if he or she is below eighteen years.

The Constitution also should protect the rights of vulnerable groups, in particular, women, children and persons with disabilities.

Also, an office should be established which is for Parliamentarians in each Constituency to see the problems of the children, young women and other people who are disabled, who cannot go to Nairobi.

You know for now, most of the offices are Nairobi, and people like the ones who are in these villages cannot get access to these parliamentarians.

Com. Ratanya: Okay, asante sana Judith. Peana memorandum yako. Twende kwa Francis Cheplait. Francis, ni wakati wako.

Francis Cheplait: Mimi naitwa Francis Cheplait, na nimesimama hapa, nataka ku-present documents mbili. Moja, inatoka kwa wakaazi wa location hii – ya Kitula Location ambayo Tambach iko chini yake. Na nyingine ambayo nita-present, ni memorandum ambayo imeandikwa na wazee wa sehemu ya Keiyo North. Basi, kama vile Bwana Chairman alikuwa amesema zamani, yangu itakuwa ni kutetea tu kidogo kidogo. Kwa hivyo naomba niruhusiwe nifanye hivyo.

Com. Ratanya: Dakika tano tu.

Francis Cheplait: Dakika tano. Asante sana Bwana Chairman. Kwanza, ni mwanzo wa Katiba. Katiba yetu, kwa sasa, inasema kuwa, Kenya ni nchi ambayo inajitawala, na inaendelea kusema mambo ya Katiba, lakini sasa, sisi tuna-propose kuwa, Katiba iseme kinaganaga kuwa, Katiba ambayo itatengenezwa wakati huu, ni Katiba ile ambayo imetengenezwa na wananchi wenyewe, yaani, itanza na, “sisi wananchi wa Kenya, tunaunda hii Katiba kwa ajili ya hii na hii”.

Ya pili, tungehitaji hiyo Katiba ionyeshe kinaganaga wakati huu kuwa, Katiba hii, ikiwi itabadilishwa kwa wakati huu, kwa sababu tunachukua muda mrefu na Wananchi wamepigania sana, Wabunge katika ule muda wa IPPG walipigania sana mpaka tumepata nafasi ya kuunda Katiba. Na tumeona hii Katiba, tumepewa nafasi hii ambayo uwezo wako chairman hiko hapo sasa, kwa sababu watu walikuwa wameona mambo mengi yakibadilika bila wananchi kuhusishwa. Kwa hivyo tungetaka leo, hasa, zile sehemu za Katiba ambazo zinahusu haki za ki-binadamu, ziwe zinakuwa referred ikiwa kuna sehemu ambayo inataka kubadilishwa. Lazima iwe referred kwa wananchi kupitia referendum.

Na zile zingine ambazo zitakuwepo, zibadilishwe na Wabunge, wakati ile vita ilikuwa katika kura, 25%. Lakini saa hii, tuna-propose ibadilishwe katika wingi wa watu Wabunge – 75% kutoka vyama vyote.

Political parties: sisi wazee wa sehemu hii, tuliona kuwa political parties ikikubaliwa kuendelea vile inaendelea sasa, tunaweza

kuwa na political parties hata pengine mia mbili ambayo mtu akikosana na mwenzake anaenda kuanza chama chake. Kwa hivyo, tungetaka political parties chache ambazo zinaweza kuwa na musimamo kamili, kama nne, ili watu wa-Kenya waweze kujiunga na yeyote kulingana na politics ya party. Sio sasa ambapo watu wanajiunga katika political parties kulingana na mtu. Tunataka tuungane, wananchi wa Kenya waungane na parties hizi, kulingana na politics ya party.

Judiciary: walisema kuwa Judiciary sasa, tuwe na courts ndogo ndogo katika vijiji ambazo zinaweza kuwa na uwezo wa kusikizwa na court ya district. Kwa sababu, wananchi wanateseka sana kwenda mahali pa court, na ambayo saa ingine inakuwa ngumu kwa wananchi kufikia.

Local Government ama structures of government: katika document ambayo sisi watu wa sehemu tulipendekeza, ni kuwa, chama ambacho kinashinda na wingi wa kura, hicho ndicho chama ambacho kitaunda serikali. Lakini, tunataka wakati watu wamejitolea kuwa ma-Rais, wajitolee kuwa ma-Rais lakini wasitoke katika constituency fulani fulani. Tunataka tu hawa watolewe na parties zao, lakini waki-run, constituency yao iwe ni Kenya. Yeye na naibu wake.

Kwa hivyo, tulionelea kuwa hiyo, itafaa na wakati imeshinda na kura ya pengine wingi wa 51%, basi hicho chama ndicho kitaunda serikali. Lakini, sisi tulionelea kuwa, tunahitaji Wabunge ambao wanachaguliwa, wawe wakifanya kazi ya Bunge na wasimamie kazi ya kamati mbali mbali za wizara. Lakini mawaziri, watoke, wateuliwe na vyama vyao, lakini watoke katika wananchi wa Kenya ambao wana uwezo wa kutosha.

Jambo lingine ambalo tulisema hapa ni kuwa, sisi wananchi wa hapa tumefurahishwa wakati mwingine. Tunachagua wajumbe, tunachagua councillors, ambao kwa muda kidogo wanaenda kwa Bunge, councillors fulani, wajumbe fulani, wanaenda huko, wanaona sukari mzuri, mzuri, wanasahau Wananchi. So, tunataka wananchi wapewe haki ya ku-recall mjumbe wao akiwa amekosa kufanya vizuri, pengine kwa muda wa miaka miwili, kupitia njia ya kumbu kumbu ya signature za wananchi, maybe 40% ya wale watu ambao waliwategua kwa constituency, ama kwa ward. Na tukishafanya hivyo,

(Interjection) Com. Ratanya: Sasa wakati wako ni kama umekwisha. Sema la mwisho.

Francis Cheplait: Basi la mwisho, nasema tukiwa hiyo re-call, tunahitaji power ya ku-recall councillors ama wajumbe kupitia njia maalum ambayo pengine itatengenezwa ili wananchi wapate nafasi ya kuwa represented kwa njia mzuri. Asante.

Com. Ratanya: Asante sana Francis. Okay, nenda uweke sahihi kwa register yetu. Na twende kwa Raymond Webor.

Raymond Webor: Asante sana Bwana Commissioner. Majina yangu ni Rayment Kiptoo Webor, na niko na mambo mawili hapa ambayo nitaenda kuzungumza juu yake.

Ya kwanza, nitaongea kuhusu mambo ya land katika nchi yetu: katika sehemu za Keiyo North, tuko na mambo ya water catchment areas. Na pendekezo letu la kwanza ni kwamba, unaona mambo ya water catchment areas, sehemu hii ambaye imefyekwa sana na imekuwa ni shida sana katika hata administration, kuangalia vile inaweza kutunzwa. Kwa hivyo, pendekezo la kwanza ni kwamba, tungetaka kamati iundwe katika kila sub-location ili wapate.....

(Interjection) Com. Ratanya: Ongea kwa hii machine hili.....

Raymond Webor: Okay, asante sana Bwana Commissioner. Nimesema, yangu itakuwa ni mambo ya land, na kwanza, ni mambo ya catchment areas. Utakuta ya kwamba, catchment areas imekuwa eneo ambalo imekuwa ikifyekwa kila wakati, na imekuwa ni ngumu sana, serikali ipate kutunza. Kwa hivyo, tumeonelea ni vizuri, committee katika kila sub-location itunzwe, ili wapate kutunza eneo hizi ambazo ni za maji.

Jambo lingine ni kwamba, tuko na mambo ya land disputes/tribunals. Nafikiri hii ni kitu ambacho kimekuwa kinachukua muda sana katika sehemu zetu. Na ningependekeza ya kwamba, ile mambo ya land dispute tribunals, iletwe mpaka sub-locational level hili watu wetu wapate urahisi kwa hizi issues za mashamba, halafu wasiwe wanaenda mpaka mbali kuchukua muda na kadhalika.

Jambo lingine ambalo ningengeza ni kwamba, hii mambo ya planning offices, ingewezekana, pia iletwe katika grassroots, hili watu wakiwa na mambo ya mashamba fulani na kadhalika, wapate kuenda haraka sana na iwafanyie kwa haraka iwezekanavyo.

